

Maombi, Ibada na Mikusanyiko Mingine Wakati wa Janga la Corona

Virusi vya Corona vinaambukiza kwa haraka sana. Wakati huu dunia inashuhudia janga kubwa ambalo linaathiri maisha ya watu, ikiwa ni pamoja na ufanyaji wa ibada, mikusanyiko na kula pamoja katika sherehe za kidini na mazishi.

Wewe ni mtaalamu na unajua namna ya kuhamasisha mabadiliko katika jamii yako. Muongozo huu utumike katika kuelewa kuhusu ufanyaji wa ibada na mikusanyiko mingine kipindi hiki cha janga la Corona:

- Tengeneza utaratibu salama ambao kila mwanajamii ataufwata. Kwa mfano, sehemu nyingine kuna wakati watu wanaimba nyimbo za kuhamasisha umoja na kupiga kelele au vyombo vya muziki. Hii huwafanya watu wajihisi kama wako pamoja japo ki uhalisia hawawezi kusogeleana.
- Kama una afya njema na hakuna mgonjwa nyumbani kwako, mnaweza kufanya matendo ya kusaidiana katika wakati huu. Hakikisha mnakaa mita 2 na mtu ambaye sio mwanafamilia.
- Dini nyingi huwa zinafanya watu wakusanyike pamoja kuzungumza au kula pamoja kama vile kufuturu ama kula daku. Kipindi hiki cha janga la Corona, watu wanaweza kuendelea kufanya hivi lakini kwa wanafamilia tu. Mikusanyiko mikubwa huchangia sana kusambaa kwa ugonjwa. Hili limetokea katika nchi nyingi na watu wameathrika zaidi.
- Shughuli za mazishi ni muhimu sana kwa kila jamii. Ila kwa wakati huu, ni muhimu sana kuchukua tahadhari wakati wa mazishi ili kuwalinda wanajamii wote. Mikusanyiko katika kufanya mazishi huongeza kusambaa kwa virusi kwa haraka sana.
- Ni muhimu kuzungumza na viongozi wa kidini na waganga wa jadi kuhusu umuhimu wa kuchukua tahadhari wakati wa mazishi kwani itasaidia sana. Jadili mambo yafuatayo na viongozi wa kidini:
 - Unachokijua kuhusu virusi vya Corona. Unaweza kuwaonesha machapisho ya iACT kama ikihitajika.
 - Namna gani tunaweza kuendelea kufanya shuguli za ibada lakini kwa kuzingatia kukaa mita 2 kutoka kwa watu wengine? Tengeneza mapendekezo pamoja nao kuhusu hili na uliza namna unaweza kusaidia kufanikisha juhudi zao.
 - Namna gani tunaweza kutoa heshima zetu za mwisho kwa waliofariki bila kuleta mikusanyiko ya wanajamii wakati wa mazishi? Ni mbinu gani tutumie ili watu wabaki salama wakati wa mazishi?
- Kama kuna dini tofauti tofauti katika jamii yako, walete viongozi wa dini hizo zote pamoja ili mjadili namna ya kushirikiana kufanya maamuzi haya muhimu. Wakati wa kikao, hakikisha mnakaa mita 2 kutoka mtu mwingine na mnavaa barakoa au kitambaa kuziba midomo na pua zenu.

Ujumbe Muhimu Kutoka kwa Viongozi Wetu wa Dini Duniani:

“Kusimamisha sala za pamoja katika masjid na shughuli nyigine za sala ni muhimu sana kwa kuzingatia malengo mazima ya Shari‘ah, na pia sio dhambi kufanya hivyo ila ni dhambi kutimiza Shari‘ah huku ukiwaweka wengine katika hatari. Malengo makubwa ya Shari‘ah ni kulinda uhai; na kusimamisha ibada za pamoja sio kusimamisha sala, (sala ni wajibu wa mtu) lakini sala za pamoja (kulingana na wajuzi wengi) sio wajibu wa mtu, mtu huweza kusali hata akiwa mwenyewe. Kusitisha sala za pamoja kutaendelea hadi wataalamu wa afya watakapotoa maelekezo kwamba watu wanaweza kusali pamoja kama zamani. Hili ni swala la kitaalamu, sio swala la kidini.

- Baraza la Fiqh la Marekani

“Katibu Mkuu wa WCC [Baraza la Makanisa Duniani] Mchungaji Dr. Olav Fykse Tveit na modereta wa kamati kuu Dr. Agnes Abuom waliwaasa watu na makanisa kuzingatia “kufanya kila ambacho kinawezekana kulinda uhai wa waumini wao” na “kuyataka makanisa kutokukusanya watu kwa ajili ya ibada...kwa kuwa kufanya hivyo ni kitovu cha kusambaza maambukizi ya virusi vya corona” na kufwata ushauri wa mamlaka na wataalamu zinatoletwa na Shirika la Afya Duniani (WHO). - Baraza la Makanisa Duniani

“Lazima tukumbuke pia kwamba hakuna ambaye anaweza kuyakwepa mateso hivyo tuwasaidie wengine wasio na makazi au familia na kuwalinda. Janga hili linatukumbusha kwamba sisi ni wamoja –hata pale tunapojiona tunaishi sehemu tofauti tofauti. Hivyo, wote tuna jukumu la kuonesha huruma na kusaidia...natumaini kwamba kila mmoja atabaki salama na kwa utulivu. Katika kipindi hiki kigumu, ni vyema kutokukata tamaa na kupoteza matumaini na ujasiri katika juhudi za kujenga zinazofanya na watu wengi duniani ili kusaidia kupunguza na kuondoa ugonjwa huu wa Corona” - Dalai Lama

“Moja kati ya misemo ya kiafrika ni kwamba “kidole kimoja hakiwezi kuchota unga”. Kwa hiyo tuungane kuondoa hili janga linalotesa watu katika nchi zetu na dunia kwa ujumla. Corona imeleta athari mbaya sana kiafya, kiuchumi na kijamii na hata kiroho. – Kadinali.”

- Philippe Nakellentuba Ouédraogo